

12. Notes from the Underground

12. Notes from the Underground

Karibu kwenye muhtasari wa kitabu cha KUMI NA MBILI kwenye orodha ya vitabu 100 ninavyosoma kwa siku 100.

Notes from the Underground ni riwaya iliyoandikwa na Feodor Dostoevsky ambapo mtu anasimulia maisha yake ambapo anaeleza siri kubwa ambayo amekuwa anajificha hata yeye mwenyewe.



Msimuliaji anaanza kwa kueleza ni mgonjwa, muovu na asiye na mvuto.

Anaamini ini lake lina shida, lakini hataki kwenda kwa daktari.

Siyo kwamba hajui au kuheshimu umuhimu wa madaktari, anaeleza ni msomi mzuri, ila hataki tu kwenda kwa daktari.

Anaeleza amekuwa na ugonjwa huo kwa miaka 20, sasa ana miaka 40.

Amewahi kufanya kazi serikalini, ila kwa sasa ameacha.

Anaeleza wakati akiwa mfanyakazi wa serikali alikuwa na roho mbaya kazini, raha yake kuona wengine hawana furaha.

Kilichokuwa kinamfanya awe na roho mbaya ni kuona kama wengine wako juu yake, wanayafurahia maisha kuliko yeye.

Anaeleza alijiona hawezi kuwa chochote na yeyote anayeamini anaweza kuwa chochote ni mpumbavu.

Anaeleza kuchagua kuwa chochote ni kujiwekea ukomo kwenye maisha.

Anaeleza hivyo ndivyo amekuwa anaamini kwa miaka 40 ya maisha yake.

Ma anaamini miaka 40 ni mingi sana, ndiyo mwisho wa maisha ya wenye akili.

Anaeleza woto wanaoishi zaidi ya miaka 40 hawana akili wala maadili.

Pamoja na hayo, anaamini ataishi zaidi ya miaka 40, zaidi hata ya 60.

Anaeleza kwamba alikuwa anafanya kazi serikalini ili tu apate pesa ya kula.

Mwaka uliopita ndugu yake amefariki dunia na kumwachia urithi, hivyo akaamua kuacha kazi na kuamua kukaa ndani bila kutoka, huku msaidizi wake akiwa mwanamke mzee.

Anasema aliambiwa hali ya hewa ya Petersburg siyo nzuri kwake, lakini ameamua atabaki hapo, hataenda pengine popote.



Msimuliaji anaeleza kwamba kitu pekee kinamchomzuia asichague kuwa mtu wa aina fulani ni kufikiri sana.

Anaamini kufikiri sana ni aina ya ugonjwa, na kwa kuwa kuendesha tu maisha ya kawaida tayari kunachukua nusu ya fikra za mtu, kuchagua utakuwa mtu gani kutapelekea mtu afikiri sana.

Anaeleza jinsi amekuwa akiendesha maisha yake kwa kuangalia sheria za asili, maana hizo hawezi kuzipinga wala kubishana nazo kwa kuwa haziangalii maoni ya watu.

Pia anaeleza jinsi watu wanavyopenda kujisifia kwa magonjwa waliyonayo, ni kama mtu anapata ufahari kwenye kile kinachomtesa.

Anaeleza pia wakati mwingine anavyotamani hata mtu ampige, kwa kuwa maumivu kwake na hata kwa wengine ni kitu anachofurahia.



Msimuliaji anaongelea kuhusu kulipa kisasi,

Anaeleza jinsi watu wanavyoweka moyoni yake waliyofanyiwa na kupanga kulipa kisasi.

Lakini anaeleza hilo ni jambo la kijinga sana kufanya, kwani anayelipa kisasi ndiye anayeumia zaidi kuliko anayemlipia kisasi.

Anaeleza jinsi watu wengi wanavyojisumbua na mambo madogo ambayo baadaye huwatesa. Anaendelea kusisitiza umuhimu wa kukubaliana na sheria za asili na kanuni za hisabati. Kama mbili jumlisha mbili ni nne, ni ujinga kutaka kubisha hilo. Kama umekutana na ukuta, ni kujiumiza mwenyewe kama utasukuma kichwa chako kwenye ukuta huo.

👉4

Msimuliaji anaeleza mtu anaweza kupata raha kwenye kitu chochote kile. Anachukulia mfano wa maumivu ya jino, ni maumivy makali kweli, lakini mtu anapata raha kwenye maumivu hayo pale anapoyaugulia. Kwa mtu kuugulia maumivu yake, anawafanya wengine wasijisikie vizuri na hilo linampa raha. Yaani mtu anafurahia pale anapoona haumii mwenyewe. Mwandishi anasema hiyo ndiyo raha pekee watu wanaipata kwenye maumivu, maana isingekuwa raha, watu wasingekuwa wanafanya hivyo. Maana maumivu yanaendelea kuwepo, iwe unaugulia au huugulii, hivyo kuugulia hakubadilishi chochote kwenye maumivu aliyonayo mtu. Lakini watu wanaugulia maumivu, kwa sababu kuugulia kunafanya wengine nao waumie na hilo linawapa raha kuona hawaumii peke yao.

👉5

Msimuliaji anaeleza hajaweza kuwa chochote kwa sababu pia hajaweza kufanya chochote. Anaamini ili mtu aweze kufanya chochote, lazima kwanza akili yake iwe imetulia, kwa kuwa na uhahika na kile anachokwenda kufanya. Anaamini ni mpumbavu pekee anayeweza kuwa na uhakika na utulivu wa aina hiyo, maana anakuwa amejiwekea ukomo kwenye akili yake. Lakini kwake yeye, akili yake haina ukomo na hivyo amekuwa hawezi kupata utulivu wa kuamua kufanya jambo fulani. Anaeleza hata kwenye kulipa kisasi, lazima mtu aamini anafanya hivyo kwa ajili ya kupata haki yake, kitu ambacho huwa hakitokei.

👉6

Msimuliaji anaeleza kama angekuwa hafanyi chochote kwa kuwa ni mvivu, hilo lingekuwa ufahari kwake. Kwa sababu angekuwa amechagua kuwa mtu wa aina fulani, mtu mvivu na watu wangemjua kwa hilo. Anaeleza angeweza kujisifia kwa hilo, kama wengine wanavyojisifia kwa ulevi au mengine wanayojulikana kwayo. Lakini yeye hata uvivu hauwezi, hana chochote anachojulikana nacho, ambacho wengine wanaweza kumwita huyu ni mtu fulani au mtu wa aina fulani.

👉7

Msimuliaji anaeleza imekuwa inaaminika kwamba watu hufanya uovu pale wanapokuwa hawajui nini wanachotaka. Kwamba mtu akishajua kile anachotaka, hatapoteza muda kwenye mambo yatakayomzuia kukipata. Lakini hii siyo kweli mara zote, watu wanaweza kujua vizuri kabisa wanachotaka, lakini bado wakachagua kufanya mambo yanayoingilia kile wanachotaka. Hapa msimuliaji anaeleza ni jinsi gani watu ni wapumbavu, walivyo tayari kufanya chochote, hata kama kina madhara kwao. Anaendelea kueleza kwamba wachumi na wanatakwimu wanekuwa wanasema watu wanataka mafanikio, mali, utulivu na amani. Lakini kuna kitu kimoja ambacho watu wanakitaka sana ila hakijawekwa kwenye orodha hiyo, kitu hicho ni UHURU WA KUCHAGUA. Uhuru wa kuchagua ndiyo hutaji namba moja kwa kila mtu, na watu wapo tayari kufanya chochoye ili

kupata uhuru huo.

Msimuliaji anaeleza pia jinsi watu wamekuwa wakiamini maendeleo ya sayansi yatawafanya watu kuwa bora na kuacha ukatili ambao umekuwepo miaka ya nyuma.

Lakini hilo halijatokea, licha ya sayansi kupiga hatua kubwa, bado watu wana ukatili wa zamani.

Akieleza kwenye karne ya 19, bado watu walipenda vita licha ya kila mtu kujua madhara yake.



8

Msimuliaji anasema anajua mtu utapinga, kwamba hitaji kuu la kila mtu ni UHURU WA KUCHAGUA, kwa kuwa mara nyingi imeonekana watu hawawezi kuchagua kilicho sahihi kwao.

Anaeleza kuchagua kunaathiriwa na mambo mawili, fikra na hisia, wengi husukumwa na hisia kuchagua kile ambacho kifikra hakina manufaa kwao.

Laki msimuliaji anaeleza kile anachochagua mtu, iwe kina manufaa au hakina ni njia ya kutaka kuonesha uhuru wake.

Anaeleza unaweza kumpa mtu kila anachohitaji, kazi yake iwe ni kula, kulala na kuzaliana tu, lakini ataishia kufanya jambo la hovy linalopoteza hata yale aliyopata.

Siyo kwa sababu mtu huyo hawezi kufikiri na kuona faida na hasara za kitu, ila kwa sababu mtu huyo anataka kuonesha na kuthibitisha yeye ni mtu mwenye maamuzi yake.

Hivyo msimuliaji anaendelea kusesitiza kwamba hitaji kuu la kila mtu ni UHURU WA KUCHAGUA na hata kama atapewa kila anachotaka, yuko tayari kupoteza hayo ili tu kuonesha yuko huru kuchagua.

Hapo unaweza kuelewa kwa nini watu wanaweza kufanya maamuzi ambayo kwa nje yanaonekana ni ya hovy kabisa, ndani yao yanaweza kuwa na maana kubwa.



9

Msimuliaji anauliza kwa nini watu wanaamini maendeleo ya sayansi yatawapa watu uhakika na kuwaondolea mateso?

Kuna uhakika gani kwamba watu wanataka uhakika na kutokuwa na mateso?

Kwa sababu ukiyaangalia maisha ya mwanadamu, vitu hivyo viwili ndiyo vinamsukuma kuishi, kutokuwa na uhakika na mateso.

Umuhimu wa kutokuwa na uhakika kunaonekana kwenye maisha ya kila siku. Mtu anaweza kujisukuma sana kupata kitu fulani, lakini akishakipata hakifurahii, anahamia kwenye kuhangaika na kingine.

Hiyo inaonesha jinsi tusivyotaka uhakika na kutaka hali ya kutokuwa na uhakika. Kabla hujakipata kitu unafurahia mchakato wa kukifikia, ukishakipata hukifurahii tena kwa sababu tayari una uhakika nacho.

Mateso ni kitu kingine ambacho watu wanakitaka sana kwenye maisha.

Msimuliaji anaeleza ugonjwa mkubwa wa wanadamu ni kuwa na utambuzi, lakini hakuna aliye tayari kuuacha utambuzi huo.

Utambuzi wa mwanadamu ndiyo unamletea kila aina ya mateso, kwa sababu hata awe kwenye hali nzuri kiasi gani, haachi kufikiria hali mbaya ambayo amewahi kuwepo au anayoweza kuja kupitia baadaye.

Hivyo hata kama mtu hayupo kwenye mateso sasa, akili yake inafanya kazi ya kutengeneza mateso kwa ajili yake.



10

Msimuliaji anaeleza jinsi ambavyo watu hukosa shukrani kwa kile kinachowafaa kwa sababu wanafikiria vikubwa zaidi.

Mfano kama mtu ana ndoto ya kukaa kwenye hekalu, hatashukuru kibanda cha kuku kulichomzuia asinyeshewe na mvua.

Matamanio makubwa wanayokuwa nayo watu yanawafanya wakose shukrani kwa vitu vidogo vyenye manufaa kwao.



11

Msimuliaji anaeleza hizo ndiyo sababu zilizopelekea achague kutokuwa yeyote wala kutokufanya

chochote.

Badala yake akaamua kukaa mafichoni kwa miaka 40 na sasa ameamua aandike kumbukumbu zake katika kipindi hicho.

Anaeleza kuna kumbukumbu ambazo mtu hasemi kwa kila mtu ila marafiki zake, halafu kuba kumbukumbu ambazo mtu hawaambii marafiki zake ila anakuwa nazo mwenyewe na pia kuna kumbukumbu ambazo hata mtu wenyewe anazikwepa.

Anaeleza anaandika siyo kwa sababu ya wasomaji, bali kuweza kuzitoa kumbukumbu zilizojificha kwenye akili yake.

Anaeleza mtu akichagua kuandika kwa ajili ya wasomaji hawezi kueleza ukweli kama ulivyo, hasa kwa kumbukumbu zake binafsi.

Hivyo yeye haandiki kumbukumbu zake kwa ajili ya wasomaji, bali kwa ajili ya kuzitoa kwenye akili yake, maana zimejificha hata kwake mwenyewe.

👉12

Msimuliaji anaeleza jinsi maisha yake yalivyokuwa akiwa na miaka 24.

Alikuwa anafanya kazi ambayo haipendi na hakuwa anajipenda yeye mwenyewe.

Hilo lilipelekea kutokuwa na marafiki, muda mwingi kuwa mpekwe.

Kwa kuwa alijidharau mwenyewe, aliona wengine pia wanamdharau.

Kuna kipindi alikuwa anaamua haongei na mtu na kipindi kingine anafikiria kuongea na kila mtu na hata kujenga nao urafiki.

Mara kwa mara alikuwa akipatwa na sonona hivyo hakuwa akijichanganya na wengine.

Muda mwingi alitumia akiwa peke yake na kusoma sana vitabu, japo kuna wakati hilo lilimpa hofu kwa kuwa alikuwa mpweke sana.

Akaanza tabia ya kutoka usiku kutembea ili tu kuona watu wanafanya nini.

Usiku mmoja aliona watu wanapigana kwenye nyumba ya michezo na mmoja kurushwa dirishani.

Alitamani sana yeye ndiye angekuwa amerushwa dirishani, hivyo aliamua kwenda kwenye nyumba ile.

Akaamua kusimama kwenye njia ili yeyote atakayemsumbua aanzishe naye ugomvi, wapigane na arushwe dirishani.

Akiwa amesimama hapo, anakuja mwanajeshi ambaye anataka kupita, anamnyanyua na kumweka pembeni kisha kupita.

Kitendo hicho kinamuumiza sana, mwanajeshi huyo amemuonesha dharau kubwa, anajiambia atalipa kisasi.

Anafikiria njia gani ya kulipa kisasi, anafikiria kumwandikia barua ya kumtaka amuombe radhi kwa kumdhalilisha la sivyoy wapambane.

Lakini anafikiria jinsi mwanajeshi yule alivyo na mwili mkubwa, huku mwili wake ukiwa mdogo anaona ataumizwa.

Anaamua awe anatembelea maeneo ambayo mwanajeshi yule huenda, ili amuone akiwanyenyekea wengine. Kweli anaenda na kumuona jinsi ananyenyekea wale waliomzidi cheo, hilo linamfanya afurahi kidogo.

Lakini bado akikutana naye, anajikuta anakaa pembeni apite kwanza, huku mwanajeshi huyo akionekana kutokujali chochote kuhusu yeye.

Hilo linazidi kumpa hasira na kutaka alipe kisasi kitakachomfanya mwanajeshi huyo amtambue na kumpa heshima.

Anapanga siku watakayokutana njiani, hatampisha, ataenda mpaka wagusane bega kwa bega.

Lakini ili mwanajeshi huyo amheshimu, anaona anapaswa kuwa na mavazi ya heshima, ila fedha hana. Anaenda kukopa kwa bosi wake kwa kuandika akatwe mshahara wake, ananunua mavazi ya heshima kisha kwenda eneo ambalo mwanajeshi anakuwepo.

Siku ya kwanza wakiwa wanakaribiana anajikuta ameshampisha bila hata ya kufikiria, anajidharau kwa hilo na kujiambia atakuwa jasiri zaidi.

Siku ya pili wakiwa wanakaribiana, kwa hofu anajikuta ameanguka chini, mwanajeshi anampita kama hajamuona.

Anaamua aachane na mpango huo, ila anajaribu tena kwa siku nyingine, siku hiyo anajijengea ujasiri na wanagusana bega kwa bega, lakini mwanajeshi anaenda zake bila hata ya kujali. Anajiambia mwanajeshi huyo anajifanya tu lakini amemtambua na hivyo kisasi chake kimefanikiwa. Tangu hapo hajawahi kumuona tena mwanajeshi huyo kwa kuwa alihamishwa, anajiuliza huko aliko atakuwa anampuuza mtu gani mwingine.

👉13

Msimuliaji anaeleza jinsi ambavyo alikuwa na ndoto kubwa inayomsumbua kipindi hicho.

Alikuwa akijiona amepewa mamlaka makubwa ya kuwasaidia wanadamu wote.

Kwamba wanadamu wote wako chini yake na yeye ndiye anayewasaidia.

Kila alipopata ndoto hiyo alitamani sana mtu wa kuongea naye, lakini hakuwa na marafiki.

Watu pekee aliokuwa anaongea nao ni wawili.

Wa kwanza ni Anton Antonitch ambaye ni bosi wake kazini. Alikuwa akimtembelea nyumbani kwake siku ambazo siyo za kazi na kumkuta akiwa na watu wengine wakijadiliana mambo ya siasa na kazi.

Katika maongezi hayo alikuwa anaishia kuwa msikilizaji, hakuchangia chochote.

Wa pili alikuwa ni Simonov, ambaye alisoma naye. Wote aliosoma nao alishapotezana nao, lakini Simonov wamekuwa wakikutana mara moja moja. Japo maongezi yao huwa siyo ya muda mrefu.

👉14

Msimuliaji anamtembelea Simonov nyumbani kwake na kumkuta yupo na marafiki wengine wawili waliosoma pamoja.

Wanamuangalia kwa dharau wakati anaingia, kitu kinachomfanya ajisikie vibaya.

Anaona wanamdharau kwa kuwa hajapiga hatua kubwa kwenye maisha kama wengine.

Anagundua wanazungumzia kukutana pamoja na kumuaga mwenzao aitwaye Zverkov ambaye ni mwanajeshi anayeenda mbali.

Msimuliaji anakumbuka jinsi alivyokuwa haelewani na Zverkov kwa kuwa japo hakuwa na akili kana yeye, alionekana kuwa maarufu na kupendwa na wengi.

Na hata sasa Zverkov amepata vyeo vya juu jeshini.

Msimuliaji anawaambia na yeye ataenda, wanamwambia lakini alikuwa haelewani na Zverkov, anajibu ataenda ili wakamalize tofauti zao.

Baadaye msimuliaji anajiuliza ya nini amesema atashiriki, anafikiria asiende kwa sababu anajua ataenda kudhalilika.

Lakini anaona hiyo ndiyo fursa ya kwenda kujijengea heshima yake upya na pia kujenga mahusiano mazuri na wengine.

Pesa pia ni tatizo, kushiriki tukio hilo anatakiwa alipe pesa saba, yeye ana pesa 9 ya kumlipa msaidizi wake wa nyumbani.

Lakini anajiambia atashiriki, anajiandaa vizuri na kwenda kwenye tukio hilo, huku akimuacha msaidizi wake aliyekuwa anasubiria malipo yake.

👉15

Msimuliaji anawahi eneo la tukio, anafika saa 11 muda ambao walikubaliana, lakini anaambiwa muda umebadilishwa mpaka saa 12. Hilo linamuudhi, kwa nini hawakumpa taarifa ya mabadiliko?

Saa 12 inafika, wenzake wanne wanaingia. Zverkov anamsalimia kwa heshima kuliko alivyotegemea.

Simonov anamweleza alisahau kumtaarifu mabadiliko ya muda, lakini hata hivyo hajui anwani yake, hivyo hajui angetuma wapi. Simonov haonekani kufurahishwa na uwepo wa msimuliaji pale.

Zverkov anamwambia msimuliaji jinsi walikuwa hawapatani na anafurahi sasa wana banafi ya kuanza upya.

Anamuuliza anafanya kazi wapi na mshahara kiasi gani, msimuliaji anataja. Wenzake wanamcheka na kusema analipwa kidogo sana, anawezaje kuendesha maisha yake. Anawajibu kwa hasira yuko hapo kwa kujilipia mwenyewe.

Simonov na wenzake wawili wanaongea maneno ya kumdharau na kumkejeli. Msimuliaji anafikiria aondoke lakini anajiambia atakaa mpaka mwisho.

Wanakula na kunywa mpaka kulewa, kwa sehemu kubwa wamempuuza msimuliaji, ni kama vile hayupo. Hilo linamfanya ajisikie vibaya, anatamani awapige na chupa kisha aondoke, ila anaona hilo siyo sahihi, anakaa mpaka mwisho.

Zverkov anawaambia wenzake ni muda wa kuondoka, msimuliaji anawaambia ana neno kwa ajili yao, anaomba sana wampokee kama rafiki. Wanamcheka na kuondoka zao.

Simonov amebaki kulipa bili, msimuliaji anamuomba ampe pesa 6, anamjibu hana, msimuliaji anamwambia ameziona anazo na anazihitaji sana. Simonov anamwambia kama huna aibu chukua. Anaondoka na msimuliaji anajiambia atawafuata popote wanapokwenda kuhakikisha wanamuomba urafiki au atampiga Zverkov kofi.

👉16

Msimuliaji anatoka nje na hawaoni wenzake, ila anajiambia anajua walipokwenda. Hivyo anachukua usafiri kuwafuata, anamsisitiza dereva aendeshe haraka.

Akiwa njiani anafikiria jinsi atakavyowakuta na kuwataka wamuombe urafiki, kama watakataa atampiga Zverkov kibao cha dharau. Na huenda hapo wataanza kumpiga, lakini atakuwa amekamilisha hilo.

Anaendelea kufikiria labda atafanya hivyo na hawatamjibu, hawatataka kupigana naye, kesho yake atamfuata Zverkov akiwa anapanda treni na kumpiga tena.

Anaona hilo linaweza kupelekea afungwe gereza na maisha yake yote yawe yameharibika.

Anajiambia labda siyo wazo zuri kuwafuata, bora aende nyumbani. Ila anajiambia ataenda tu.

Anafika kwenye klabu ya usiku alipodhani wameenda, anaingia na kuwatafuta ila hawaoni.

Akiwa pale mwanamke mrembo anaingia, anajikuta anamuangalia lakini hapati mvuto ndani yake.

👉17

Ni saa nane usiku, msimuliaji anajikuta amelala na mwanamke kwenye chumba kilicho ndani ya ile klabu ya usiku.

Mwanamke aliyelala naye ni yule aliyemuona wakati anaingia, mpaka muda huo hawajaongea chochote.

Anamuuliza jina lake nani, anamjibu Liza, anamuuliza ametokea wapi anamjibu. Anamuuliza kama ana baba na mama, anajibu wapo. Anamuuliza ameanza mazi hapo kwenye klabu lini anamjibu siku chache zilizopita.

Msimuliaji anamuuliza kwa nini amechagua kuiacha familia yake na kuja kufanya kazi hiyo ya kujiuza. Anamwambia ni kazi itakayomlipa kwenye mwaka wa kwanza, lakini baada ya hapo thamani yake itakuwa inashuka. Na bado kuna hatari ya kupata magonjwa.

Anamwambia yeye hakupata bahati ya kuwa na familia, ndiyo maana maisha yake yamekuwa hovyoyote.

Ila akija kupata mtoto wa kike, atampenda kuliko kitu kingine chochote na hatakuwa tayari hata aolewe. Ila kama atapata mwanaume ambaye yeye binti amependa mwenyewe, hatakuwa na kipingamizi.

Msimuliaji anaendelea kueleza, msingi mkuu wa ndoa ni upendo, upendo ukishakuwepo, hata kama pesa hakuna, wanandoa wataishi kwa furaha na kuheshimiana.

Hata pale wanapotofautiana, hawataruhusu tofauti zao zitoke nje, hata wazazi hawatazijua, watazimaliza wao wenyewe na kuendelea kuishi kwa furaha.

Anasema watu husema watoto ndiyo huondoa upendo kwenye ndoa, lakini hilo siyo kweli, kwenye ndoa yenye upendo, watoto huongeza upendo zaidi. Kwani wazazi huona jinsi lilivyo jukumu lao kuwalea watoto hao vizuri.

Msimuliaji anajisikia vizuri kwa hotuba hiyo aliyoitoa kuhusu maisha na upendo.

Mwanamke yule anamuuliza mbona unaongea kama kitabu?

Msimuliaji anashangazwa, alitegemea mwanamke huyo angeshukuru kwa ushauri mzuri aliompa, ila anaona ni njia ya kuficha hisia zake.

👉18

Msimuliaji anamwambia Liza kwa sasa bado ni binti na mrembo, usidhani utabaki hivyo. Siku

zinavyokwenda utachoka na thamani yako itapungua.

Anamwambia kwa sasa tu tayari thamani yake inapungua, wanaume wanaomtaka hapo ni walevi na hawafati upendo bali ngono tu.

Anamwambia kama angekuwa binti aliyetulia kwenye familia yake, angepata mchumba wa kumuoa na akawa na maisha mazuri.

Lakini hapo amechagua maisha ya utumwa, siyo tu ameuza mwili wake, bali pia ameuza roho yake.

Anamweleza maisha yake yatakuwa ya utumwa milele, miaka michache hapo watamchoka na kumfukuza, ataenda nyumba nyingine ya kujiuza ambapo thamani yake itakuwa chini zaidi na hapo pia watamchoka na kumfukuza, mwisho ataishia kuwa kahaba wa mtaani.

Anamwambia kwa maisha aliyochagua, hata akifa hakuna anayemzika kwa heshima, na akishazikwa maisha yake yanakuwa yamefutika kabisa duniani maana anakuwa hajaacha alama yoyote.

Msimuliaji anaongea kwa hisia mpaka anajistukia, anamwangalia Liza na kukuta analia machozi, anajisikia vibaya kwamba aliyomuambia yameumiza moyo wake.

Anaamka kuondoka, anamwambia Liza amsamehe kama amemuumiza na kumwachia anwani yake, akimkaribisha amtembelee kwake.

Liza anamshukuru, kabla hajaondoka anamwambia asubiri, anaenda na kurudi na barua, anampa aisome.

Msimuliaji anaisoma barua, ni ya kijana amemuandikia Liza, akimweleza jinsi anavyompenda. Liza anamwambia msimuliaji kwamba kijana huyo hajajua kazi yake, hivyo anapanga kulipa deni alilovalo hapo kisha aache kazi hiyo.

Msimuliaji anajiambia Liza ataishi na barua ile milele kama kumbukumbu ya aliwahi kupendwa, ila kuiacha kazi hiyo itakuwa vigumu, maana ameshafanywa mtumwa.

👉19

Msimuliaji anaamka asubuhi akiwa amechoka. Anakumbuka yote yaliyotokea siku ya jana na kuona haikwenda sahihi.

Anaenda kazini na kukopa fedha kwa boshi wake, anamwandikia Simonov barua ya kuomba samahani kwa yaliyotokea jana na kuambatanisha pesa sita alizomkopa.

Anamuomba amwombee msamaha kwa wengine na kama watapata nafasi nyingine pamoja atafurahi.

Swala hilo anakuwa amelimaliza, anabaki na swala moja linamsumbua kwenye akili yake, kuhusu Liza.

Anajiambia Liza atakuja, lakini itakuwaje atakapokuja? Akiyaona maisha yake si atamdharau? Hasa akizingatia ushauri wa maisha aliompa.

Siku ya kwanza inapita, Liza hajaja, siku ya pili, ya tatu. Bado msimuliaji anamfikiria tu, anajiambia labda ananyimwa kutoka, ila anajiambia atakuja tu.

Hata akilala anajikuta anamuota Liza, wako pamoja, kama mke na mume.

Hasira za kutokuja kwa Liza anazimalizia kwa msaidizi wake anayeitwa Apollon. Ni mzee mwenye dharau na asiye jali, Msimuliaji hampendi ila hana namna ndiyo anamtegemea amsaidia majukumu yake, amekuwa naye kwa miaka saba sasa.

Kila mwezi anamlipa pesa saba na ikipita siku hajamlipa mzee huyo humwangalia kwa dharau na ukali mpaka yeye mwenyewe anaogopa na kumpa pesa yake.

Safari hii anajiambia atamfundisha somo, hatampa pesa yake mpaka aje aiombe. Siku ya kwanza inapita, mzee anaanza kumwangalia vibaya. Siku ya pili tena anafanya hivyo, msimuliaji anamwita na kumwambia najua unaniangalia vibaya kwa sababu sijakulipa, pesa yako yote hii hapa, ila sitakulipa mpaka uje uombe. Anamwambia wewe mzee ni mtesaji na una dharau, mpaka utakapokuja kwa heshima na kuomba ndiyo nitakupa mshahara wako. Apollon anamjibu hilo halitatokea, anaanza kuondoka, anamwambia usiende popote, nijibu hapa. Mzee anamwambia anaweza kumuitia polisi maana amemtukana na kumshutumu, anamuacha na kuondoka.

Msimuliaji anamfuata kwenye chumba chake, anamwambia nenda haraka ukawaite polisi, hilo ni agizo nakupa. Mzee yule anamwambia atakuwa na matatizo yake binafsi, toka lini mtu ajiitie polisi yeye mwenyewe?

Wakiwa wanabishana pale mwanamke anagonga hodi, mzee anaenda kumfungulia na kumwambia ana mgeni, ni Liza.

👉20

Msimuliaji anamkaribisha Liza, anamwambia pole amemkuta kwenye hali isiyo nzuri. Anaenda kwa Apollon na kumlipa hela yake kisha anamtuka akaleta chai.

Mzee anawaletea chai na kuondoka. Wamekaa pale, Liza kwenye kiti na Msimuliaji kwenye sofa, wanakaa kimya kwa muda.

Msimuliaji anaona aibu kwa hali ambayo Liza amemkuta nayo, Liza naye anamwambia anataka kuondoka.

Msimuliaji anamuuliza kwa hasira, nini kimekulete hapa? Nijibu nini kimekuleta.

Liza anakaa kimya. Msimuliaji anaendelea kuongea, najua kilichokuleta, ni kwa sababu siku chache zilizopita nilikupa maneno ya matumaini hivyo leo umekuja kwa shujaa wako kupata tena maneno ya kukupa matumaini.

Nikuambie wazi sina maneno yoyote ya kukupa matumaini, maisha yangu kama unavyoyaona hapa ni mabovu kuliko hata yako.

Siku nakupa maneno yale nilikuwa nimetoka kudharauliwa na marafiki zangu, nilikuwa nawatafuta nilipe kisasi, ila sikuwapata. Hivyo nilipokutana na wewe nikaona ni njia ya kulipa kisasi na kuondoa hali ya kujisikia vibaya. Hivyo yote niliyokuambia, japo ni kweli, lakini ilikuwa njia ya mimi kujisikia vizuri.

Sikukuambia kwa sababu najali chochote kuhusu wewe, wala sikukuambia kwa sababu nilitaka kukuokoa, mimi mwenyewe ni wa kuokoa.

Sasa umeniona kwenye hali yangu, umeona uhalisia wangu, sina ushujaa wowote, maisha yangu ni ya hovy kama yako.

Liza anashinda kujizuia, anainuka na kwenda kumkumbatia msimuliaji ambao kwa wakati huo machozi yalikuwa yanamtoka.

Msimuliaji anajaribu kutulia lakini bado hasira ziko ndani yako, anaona jinsi Liza amegeuka kuwa wa kumsaidia katika hali anayopitia.

👉21

Msimuliaji bado ana hasira, ameenda kwenye chumba chake ila bado Liza amekaa pale, anatamani sana aondoke ila haondoki.

Anamfuata na kumwekea fedha kwenye mkono wake kisha kumfungulia mlango aondoke.

Anarudi kukaa kwenye kona ya chumba chake, ambayo anaita ni ulimwengu wake.

Liza anamuaga na kuondokaa anaiacha fedha ile pale, Msimuliaji anatoka kumfuata, anakimbia akimuita jina ila hampati.

Anajiuliza anamuita ya nini? Hata akimkuta, atafanya nini?

Anarudi ndani kwake kwenye ulimwengu wake na kujiambia hawezi kumpenda Lizi, dhana ya mapenzi kwake ni kumtisha na kumtawala mwingine.

Anajiambia ulimwengu wa kawaida haumfai, ndiyo maana ameachana nao na kuingia kwenye ulimwengu wake wa mafichoni (Underground world)

Tangu hapo hajawahi kumuona tena Lizi wala kumsikia, amechagua kuishi kwenye ulimwengu wake huo.

Anasema japo unaweza kuyadharau maisha yake, lakini jichunguze mwenyewe, kuna siri za maisha yako ambazo hata wewe mwenyewe hutaki kujiambia.

Anasema hivyo ndivyo wanadamu tulivyo, tunakuja kwenye hii dunia tukiwa na changamoto mbalimbali, tunajaribu kutumia njia tunazoweza katika kukabiliana nazo, muhimu ni kutokuyaigiza maisha, kuyaishi kwa uhalisia.

👉SOMO

Riwaya hii ambayo ni simulizi, ina menngi mno ya kutufundiaha kuhusu maisha.

1. Kikubwa kabisa ni siri ambazo kila mmoja wetu anazo, za mambo ambayo tumewahi kufanya

ambayo hata sisi wenyewe hatutaki kuyakumbuka. Kwa sehemu kubwa inakuwa imechangiwa na chuki ambazo zinakuwa ndani yetu.

2. Tumejifunza pia kulipa kisasi kusivyokuwa na manufaa yoyote, zaidi ya kumuumiza zaidi anayelipa kisasi. Unaweza kuhangaika kulipa kisasi kwa mtu ambaye hata hajui uwepo wako.

3. Tunapaswa kuzijua sheria za asili na kuzifuata bila ya kuzikataa au kubishana nazo, maana asili haijali chochote kuhusu sisi, inaenda kwa namna yake.

4. Upendo wa kweli ndiyo msingi wa mahusiano yanayodumu na yenye furaha kwa wahusika.

5. Tumejifunza hitaji kubwa la kila mtu ni uhuru wa kuchagua, mtu hata apewe kila kitu anachotaka, kama hana uhuru huo wa kuchagua yupo tayari kupoteza kila alichonacho ili tu kupata uhuru huo.

6. Kila mmoja wetu ana udhaifu ulio ndani yake, udhaifu huo ni ugonjwa ambao mtu anakuwa nao maisha yake yote, asipoutambua utakuwa kikwazo kwake kuwa na maisha anayoyataka.

7. Binadamu huwa tunataka sana uhakika kwenye kitu, ila tukishaupata tunaachana nacho na kuhangaika tusivyokuwa na uhakika navyo. Ndiyo maana wengi hulalamika mafanikio hayaleti furaha, wasichojua furaha inapaswa kuwa kwenye mchakato na siyo kusubiria mpaka matokeo.

8. Waonee huruma wanaojaribu kukuumiza au kukufanyia ubaya, ni kwa sababu tayari wanaumia na wana ubaya ndani yao. Pia kuwa makini maumivu uliyonayo usiyapeleke kwa wengine kama njia ya kujisikia vizuri.

9. Shukrani ni muhimu kwenye maisha, haijalishi una ndoto na mategemeo makubwa kiasi gani, usidharau kidogo kinachokusitiri leo.

10. Pamoja na changamoto za maisha, hatupaswi kuyakimbia, badala yake tunapaswa kuyakabili ili kuyaishi. Unapoyakimbia maisha au matatizo, huyafanyi kuwa rahisi, bali magumu zaidi.

Kwa msimuliaji kuyakimbia maisha hakujayafanya maisha yake kuwa bora, kwani anaona kila mtu ni adui au mshindani wake, hivyo anashindwa hata kukubali wale wenye mapenzi ya kweli kwake.

Wapo watu wengi wanaotupenda na kutukubali vile tulivyo, wajibu wetu ni kupokea upendo wao na sisi kuwapenda pia. Tunapokuwa watu wa kujihami muda wote, tunashindwa kuyaishi maisha bora kwetu.

Muhtasari huu umeandaliwa na Kocha Dr Makirita Amani,

www.t.me/somavitabutanania